

SIKU ZOTE MPUMBAVU YU SAHIHI MACHONI PAKE MWENYEWE

Mithali 12:15 yasema. "Njia ya mpumbavu imenyooka machoni pake mwenyewe: bali ye ye aliye na hekima husikiliza shauri." Tukingalia wanaotuzunguka, twaona kwamba watu wamekuwa wageni katika imani zao, hasa inapokutokea kwa wale wanaojiona kuwa na hekima, wakati katika uhalisia ni wapumbavu. Benjamin Franklin alisema, "Mpumbavu msomi huandika upuuzi wake katika lugha bora kuliko asiye msomi, lakini bado ni upuuzi." Neno "mpumbavu" na uwingi wake "wapumbavu hupatikana katika mistari 113 katika Biblia. Katika Agano Jipy, yapo maneno tofautitofauti yaliyotafsiriwa "mpumbavu, kwa upumbavu" au "upumbavu". Maneno haya huzungumzia wale wasio "na uwezo wa kuchunguza" "wasio na uelewa" "wasio kitu kichwani, wavivu; na hivyo, ni washenzi, wapumbavu," "wasio na upambanuzi," "kufanya upumbavu," "uwenda wazimu" na "upunguani".

Bila shaka maishani mwetu sote tumewahi kukumbana na mtu wa jinsi hii wakati fulani. Mtume Paulo aliwashughulikia waliojiona "wenye hekima" wakati katika hali halisi walikuwa ni wapumbavu (1 Wakorintho 1:20-25). Katika makala hii, tunataka kuwatazama wale wajionao wenye hekima wakati katika hali halisi ni wapumbavu.

Hata hivyo, hebu tuweke sawa jambo fulani kabla hatujafanya hivyo,. Tunachojadili hakipingamani na maneno ya Yesu katika Mathayo 5:22. Hapa Yesu alikuwa anamzungumzia mtu amwonaye mwenzake kuwa hafai. Hakuzungumzia mtu amwonaye mwenzake kuwa "mpumbavu" kutokana na matendo yao ya kipumbavu. Kama ndivyo, angebakia anajihukumu mwenyewe kutokana na mfano wa "tajiri mpumbavu" unaopatikana katika Luka 12:16-21. Katika kutafakari juu ya "mpumbavu" kwa kadri ya neno la Mungu, hatujaachwa bila uwezo wa kumjua aliye mpumbavu. Kwa kumjua mwanadamu ndani na nje, Mungu aweza kuwatambua wale ambao ni "wapumbavu" (Waebrania 4:12,13). Hatuwezi kukosea kujua maadamu tunalitazama Neno lake ili kujua mpumbavu ni yupi.,

ASEMAYE HAKUNA MUNGU NI MPUMBAVU, INGAWAJE ANAJIONA MWENYE HEKIMA-Mwimbaji wa zaburi alieleza, "Mpumbavu amesema moyoni mwake hakuna Mungu; wameharibu matendo yao na kuyafanya chukizo, *hakuna atendaye mema*" (Zaburi 14:1).

Tazama mistari ya 1-3 katika zaburi hii, inaeleza kuwa mtu wa jinsi hiyo ni chukizo na amepotoka. Walakini, kwa nini Mungu anasema mtu huyu ni mpumbavu? Kwa sababu anadai kwamba hakuna Mungu. Kwa nini anatoa madai kama hayo? Ni dhahiri kwamba si kwa sababu ya kukosekana kwa ushahidi wa uwepo wa Mungu (Zaburi 19:1). Na badala yake ni kwa sababu hivyo ndivyo anavyotaka kuamini, kuamini kuwa yuko sahihi. Wanaotaka kuishi kinyume na Mungu anavyotaka hutaka kuwa kusingekuwa na Mungu. Wenye dhambi hutaka Mungu asingekuwepo, ili asiwepo wa kuwawajibisha kwa matendo yao.

AZITUMAINIYE NJIA ZAKE NI MPUMBAVU, INGAWAJE ANAJIONA MWENYE HEKIMA.- Mtu huyu hutegemea maamuzi yake mwenyewe ili kuondokana na matakwa ya Mungu (Mithali 12:15). Kwa nini mtu huyu ni mpumbavu?

Kwa sababu moyo wa mwanadamu hukosea (Mithali16:25; Yeremia 10:23; Warumi 1:22).

Kwa sababu hukataa kumtukuza Mungu,na ni upumbavu kumwamini Mungu bila kumheshimu kama Mungu (Warumi 1:21)

Kwa sababu moyo ni mdanganyifu, na hauwezi kutumainiwa (Yeremia 17:9; Mithali 12:15).

MTU MWENYE CHOYO NI MPUMBAVU, INGAWAJE ANAJIONA MWENYE

HEKIMA- Tazama mfano katika Luka 12:13-21. Kwa nini mtu huyu alionekana kuwa mpumbavu? Kwa sababu alikuwa ni kipofu wa chanzo cha utajiri (1 Wakorintho 10:26; 1 Timotheo 6:17). Unaposoma fungu hili la mfano juu ya mtu tajiri, zingatia kwa makini kiwakilishi kilichojirudiarudia “ni”. Ni Mungu aliyeiwezesha asili kutoa mazao na wanadamu kutumika kama mawakili (1 Petro 4:10). Mtu anayeongelewa katika Luka 12, alidhani baada ya kuvuna,utajiri ungekuwa faraja. Badala yake ukawa mzigo. Alijivuna juu ya wakati ujao, ingawa hakuwa na maamuzi juu ya wakati ujao kama inavyoonekana katika maelezo yake “Nita” (Luka 12:18,19). Angekuwa na tabia kama inavyoonekana katika Yakobo 4:13,14

ASIKIAYE LAKINI HATII NI MPUMBAVU, INGAWAJE ANAJIONA MWENYE

HEKIMA – Tafakari kwa makini maneno ya Yesu katika Mathayo 7:26,27. Kwa nini huyu ni mpumbavu? Jibu ni jepesi, kusikiliza hakufai, kusipofuatiwa na utii (Yakobo 1:22-25). Anayesikiliza simu za tahadhari, lakini akashindwa kuzingatia, kwa vitendo kama hivyo huonyesha ukosefu wa hekima wazi wazi.

ASIYEJIANDAA KWA AJILI YA HUKUMU NI MPUMBAVU, INGAWAJE

ANAJIONA MWENYE HEKIMA –Angalia kwa makin maneno ya Yesu yanayopatikana katika Mathayo 25:1-13. Kwa nini wale wanawali watano walielezewa Kwamba walikuwa wapumbavu? Ni kwa sababu waliishi kwa ajili ya maisha yaliyopo, na hawakujali kilicho mbeleni. Walisahahu tahadhari ya kuwa tayari. Walijaribu kutafuta kimbilio kwenye fomu, taa, vyombo, na majina. Walipuuza kwamba mafuta yalihitajika kwa ajili ya taa zao.

Tujihadhari ili tusionekane wapumbavu machoni pa Mungu